CHATO COLLEGE OF HEALTH SCIENCES AND TECHNOLOGY

P.O. Box 73, Chato – Geita – Tanzania

Tel: +255 784 638 495 / +255 767 150 048 / +255 763 759 363/ +255 752 180 914

Website:www.chatocollege.ac.tz: email: chatocohest@gmail.com

Kumb.Na:HAS.158/05/2022 **Tarehe: 27/07/2023**

KWA NDUGU:

.....

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO KATIKA CHUO CHA SAYANSI YA AFYA NA TEKNOLOJIA-CHATO

Napenda kutumia nafasi hii kukupongeza na kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na mafunzo katika Chuo cha Sayansi ya Afya na Teknolojia-chato kilichopo Mkoa wa Geita, Wilaya ya Chato katika kozi ya Stashahada ya Teknolojia ya habari na mawasiiano **(Ordinary diploma in information and communication technology)** kwa muda wa miaka **mitatu** kwa mwaka wa masomo **2023/2024.**

Kwa barua hii unatakiwa kuripoti chuoni siku ya Jumatatu **tarehe 28/08/2021 tayari kwa kuanza masomo** kuanzia saa 2:00 asubuhi mpaka saa 10:30 jioni kwa ajili ya usajili ambapo masomo yataanza tarehe **04/10/2023.**Ikumbukwe kuwa kama hautafika katika muda uliotajwa hautapokelewa na nafasi yako itajazwa na mtu mwingine.

Chuo kina Hosteli za kutosha kwa wanaume na wanawake, hivyo wanafunzi wote wanapaswa kuishi ndani ya Hostel kwa kusudi la kulinda nidhamu na usalama wao.

1. **MALIPO**

- Ada za kozi ya Information and communication technology (ICT) ni **Tsh. 500,000/= (Laki tano tu)** kwa kila mwaka mmoja wa masomo,malipo haya hayajumuishi ghalama za chakula na michango mingine.

- Huduma ya Hostel inapatikana hapa chuoni bila malipo yoyote (bure)na nivyema wanafunzi wote waishi ndani ya Hostel za Chuo ili kuwezesha wanafunzi kupata malezi ya

kimaadili kwa kuzingatia Haiba ya Utumishi wa taaluma ya kada ya Afya.

- Chuo kina utaratibu mzuri wa Chakula hapahapa chuoni kwa Gharama ya Tshs **350,000/=** kwa muhula mmoja wa masomo malipo ambayo ni sawa na kiasi cha Tsh 2,100/= kwa siku moja yenye milo mitatu,malipo ya chakula yanalipwa kila mwanzo wa muhula wa masomo unapoanza ili kufanya maandalizi ya chakula. Kwa kuzingatia malezi na maadili ya taaluma za Afya ni sharti mwanafunzi apate huduma zote ndani ya chuo kwa kuzingatia maelekezo hapo juu malipo yote ya chakula yalipwe kupitia

  Akaunti namba **31010028074 (NMB)**yenye **jina la SAFLOCA GROUP.**

- Kama mwanafunzi hana kadi ya mfuko wa taifa wa Bima ya Afya ni lazima Alipie kiasi cha Tshs=**54,000/**= mara tu afikapo chuoni ili mwanafunzi huyo aanze kuandaliwa mchakato wa kupata kadi ya Bima ya Afya (NHIF) itakayomwezesha kupata matibabu ngazi zote za hospitali zinazohudumia wanachama wa mfuko huo wa serikali na inalipwa kwa kila mwaka unapoanza.

UTARATIBU WA MALIPO YA ADA PEKEE

1. Malipo ya Ada pamoja na michango mingine ya Chuo yafanyike kwenye akaunti ya chuo kupitia Benki ya **NMB** akaunti Namba. **32710008227** Jina la akaunti ni **CHATO COLLEGE OF HEALTH SCIENCES AND TECHNOLOGY,au CRDB A/C Na.0150426444500 Jina Chato College of Health Sciences and Technology,Tofauti na michango mingine iliyotajwa katika jedwali la maelekezo.**

2. Malipo ya umoja wa wanafunzi shilingi **20,000** yafanyike kupitia Benki ya **NMB** akaunti Namba **32710021476** Jina la akaunti ni **CHATO COLLEGE OF HEALTH STUDENT'S ORGANIZATION na stakabadhi ya banki iwasilishwe kwa mhasibu wa chou.**

3. ***KUMBUKA kutochanganya malipo haya pamoja na malipo ya Ada ya Chuo. Chuo hakitakuwa na mamlaka ya kutatua tatizo hili iwapo utachanganya malipo haya ya wizara ya Afya.***

Unasisitizwa kuripoti mapema ili taarifa zako ziingizwe kwenye mfumo wa udahili na ziweze kutumwa NACTE kwa muda uliopangwa ili kuepusha usumbufu. Hakikisha unakuja na picha (4) za rangi

(passport size) zilizopigwa hivi karibuni.(Current passport size) pamoja na vyeti halisi kwa ajiri ya uhakiki.

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

(i) Hatupokei fedha taslimu chuoni za ADA wala kwa njia ya Simu,Ukitaka kulipa kwa njia ya simu tupigie simu ili upewe namba ya malipo(**CONTROL NUMBER)** mfumo uingize malipo hayo kwenye akaunti husika ya mwanafunzi ambapo hutalazimika kuleta risiti ya malipo. Malipo yote yafanyike kupitia Benki tu ikiwa ni pamoja na malipo umoja wa wanafunzi na malipo ya chakula yatalipiwa kupitia Akaunti namba kama ilivyoonyeshwa hapo juu.

(ii) Hairuhusiwi kupika hostel wala kuonekana na jiko, pasi au vyombo vya kupikia sehemu hiyo.

(iii) Hautapokelewa chuoni kama utakuja bila kukamilisha malipo na mahitaji yanayotakiwa unapofika.

MAHITAJI

Wanachuo wote wanatakiwa kuja na vitu vifuatavyo:-

- Nakala ya cheti cha kuhitimu kidato cha nne/sita na nakala ya cheti cha kuzaliwa kwa uhakiki .

- Vifaa vya kutosha vya kujifunzia kama vile Daftari (counter books) kalamu, rula n.k

- Vitabu vya rejea vinavyohusu kozi husika kama vile anatomy and physiology (ROSE & WILSON) na Medical Dictionary pindi unapokuwa mbali na maktaba ya chuo kwa ajiri ya rejea.

- Mwamvuli au koti kwa ajili ya matumizi wakati wa majira ya mvua au baridi ili kuepusha kutohudhuria vipindi kwa sababu ya mvua (Hii ni hiari na si lazima).

- Nguo na viatu vya michezo.
- Taarifa ya kupima Afya (medical examination) kutoka kwenye hospital au kituo cha Afya kinachotambulika.(Fomu imeambatanishwa na inapatikana kupitia **www.chatocollege.ac.tz**)

- Fedhaa kwa ajili ya track suit ya rangi nyeusi na misitari myeupe kwenye mikono kiasi cha Tshs 20,000/=.
- Rimu Tatu (3) za karatasi aina ya **Double A** mara tu anapofika chuoni hii ni kwa ajiri ya mitihani ya kila mwezi pamoja na ile ya kumaliza muhula.

- Mfagio wa ndani (Soft bloom) mmoja,Mfagio wa kudekia nan doo yake (Mopper) moja,Pamoja na Leki ya kukusanyia takataka kwa ajili ya usafi wa mazingira.

MAHITAJI KWA AJILI HOSTELI.

Yafuatayo ni mahitaji ambayo wanachuo wanapaswa kuja nayo kwa ajili ya Hosteli;-

- Shuka 4, Blanketi 1, chandarua cha pembe nne kinachoenea kwenye kitanda cha futi 3x6, foronya 1 na taulo 1.
- Ndoo moja ya plastic ya lita 20,ndoo moja ya lita 10 na Sanduku au Begi la kutunzia vitu vya thamani lenye kufungwa na kufuri kwa ajiri ya usalama binafsi.
- Godoro aina ya comfy au super banco la futi $2^1/_2$ kwa 6 kwa wanafunzinzi wote au fedha kiasi cha Tshs 65,000/= kwa ajiri ya kununulia godoro.

4. SARE:

Wanachuo wote watatakiwa kuja na fedha za kushona sare ili kuepusha makosa ya uchaguzi wa kitambaa na ushonaji usio wa maadili yaliyoelekezwa na wizara ya Afya,Maendeleo ya Jamii,Jinsia na watoto ambazo zitakidhi matakwa na maadili ya taaluma na jamii.Ikumbukwe kuwa nguo zinazoonyesha maumbile hazitaruhusiwa hapa Chuoni kiasi cha Tshs 70,000/=
zinahitajika kwa ajiri ya uniform za kushona yaani Gauni 2 kwa wasichana na suluali 2 kwa wavulana,koti la hospitali moja,

Pia unaweza kushona koti la hospitali kati ya 20,000 hadi 25,000/= **fedha hizi zisiwekwe kwenye akaunti na ni lazima kushona uniform kwa fundi aliyeidhinishwa.**

KOZI	AINA YA SARE
INFORMATION AND COMMUNICATION TECHNOLOGY(ICT)	✞ Mashati mawili meupe ya mikono mifupi kwa wavulana. ✞ Suruali mbili za rangi ya khaki kwa wavulana. ✞ Gauni mbili za rangi nyeupe kwa wasichana. ✞ Viatu vyeusi vya ngozi. ✞ Track Suit nyeusi na misitari myeupe mikononi. ✞ Sweta Nyeupe litakalovaliwa darasani wakati wa baridi

MATIBABU

Chuo kinatumia mfumo wa Bima ya Afya ya Taifa (NHIF) kwa kupata matibabu katika Hospitali yetu ya wilaya ambayo ndiyo Hospitali ya mafunzo kwa wanachuo wote.

ULINZI NA USALAMA

Ili kuhakikisha usalama wa mali na vitu vya Wanachuo na Watumishi , chuo kina ulinzi wa kutosha katika mazingira ya Chuo,hata hivyo wilaya ya Chato ina usalama wa kutosha kwa mazingira yote.

SHERIA NA TARATIBU ZA CHUO

Chuo kina sharia na taratibu mbalimbali zilizowekwa kwa ajili ya kudumisha nidhamu za wanachuo wakati wa mafunzo ili kusaidia kuleta maadili yaliyokusudiwa katika taaluma inayofundishwa. Chuo kinatumia sharia za Wizara ya Afya kwa ajili ya vyuo vyote vya Afya Tanzania Bara. Kwa hiyo wanachuo wote watatakiwa kuzisoma vizuri sharia hizo mara tu wafikapo chuoni na kuzizingatia siku zote. Baada ya kusomewa /kuzisoma sharia hizo kila mwanafunzi atatakiwa kusaini kopi yake na itatunzwa kwenye faili la kila mwanafunzi.

6. JINSI YA KUFIKA CHUONI

Chuo kipo eneo la Mbuye katika kata ya Bwina chato mjini wilaya ya Chato Mkoa wa Geita. *Uwapo nasi Afya imezingatiwa*.

Dr Joel Limbu.Maduhu(MD,MPH,DCM).

MKUU WA CHUO

Chato College of Health Science and Technology.

Principal
Chato College Of Health Sciences
And Technology
P. O. Box 73, Chato, Geita - Tanzania

Na	AINA YA MALIPO	KIASI (Tsh.)
1	Ada ya mafunzo (Tuition fees)	500,000/=
3	Ukaguzi wa viwango vya ubora (NACTE QUALITY ASSURANCE FEE)	15,000.00
4	Fedha ya kitambulisho	20,000.00

5	Fedha ya T-Shirt	20,000.00

KIAMBATANISHO– A

MCHANGANUO WA ADA NA MICHANGO MINGINE:

Ifuatayo ni michango mingine ambayo inapaswa kulipwa wakati wa kuripoti na hailipwi kwa awamu (inalipwa mara moja tu) isipokuwa fedha ya chakula tu inaweza kugawanywa awamu mbili.

6	Gharama ya maktaba ,Computer na usomaji mtandao	150,000.00
7	Gharama ya usajili	50,000.00
8	Gharama za ukarabati	100,000.00
9	Fedha ya tahadhali	50,000.00
10	Gharama ya mitihani ya ndani na majaribio (chuoni)	100,000.00
11	Mchango wa umoja wa wanafunzi(Student union fees)	20,000.00
12	Malipo ya Bima ya Afya (NHIF)kwa wasiokuwa na kadi ya bima ya Afya tu	54,000.00
13	Mazoezi ya vitendo	100,000.00
14	Practical procedure Books / log books	20,000.00
15	Umeme na maji	70,000.00
16	Fedha ya chakula kwa mwaka (unaweza kulipa awamu mbili au tatu yaani 300,000/=,200,000/= na 200,000/=	700,000.00
	JUMLA KUU PAMOJA NA CHAKULA	**1,969,000.00**

NB:Mchanganuo wa awamu za malipo imeonyeshwa hapa chini kwa atakayehitaji kulipa kwa awamu.

	Kozi	Awamu ya 1 (September 2021)	Awamu ya II January 2022	Awamu ya III (May,2022)	Jumla
1	INFORMATION AND COMMUNICATION TECHNOLOGY	300,000/=	100,000/=	100,000/=	500,000
2	Malipo yasio ADA(Michango mingine)	469,000	100,000/=	200,000/=	769,000
3	Chakula	300,000/=	200,000/=	200,000/=	700,000
	JUMLA	1,069,000/=	400,000/=	500,000/=	1,969,000/

CODE OF CONDUCT:

"Chato college of Health Science and Technology believes in equal opportunity and does not discriminate against any student or prospective student on the basis of race, sex, origin disability or religion. Thus, you are supposed to abide with the college rules and regulations attached to this letter and sign below if you agree and accept the offer". You are warmly welcome and I wish you God's blessings through your academic work at the centre.

KIAMBATANISHO

KANUNI NA SHERIA ZA CHUO CHA SAYANSI YA AFYA NA TEKNOLOJIA CHATO

1. Kwa miaka yote ya masomo mwanafunzi haruhusiwi kuwa na shughuli nyingine zissizohusiana na masomo yaliyomleta hapa Chuoni.
2. Ni lazima mwanafunzi afuate sheria, maadili na taratibu za jamii wakati wote wa masomo yake hapa Chuoni.
3. Kazi zisizo za lazima kama kufua, kupiga pasi n.k zifanyike Jumapili au Jumamosi isipokuwa kazi ya kutunza usafi wa mazingira.
4. Inawapasa wanafunzi wawe waaminifu daima; adhabu kali itatolewa kwa udanganyifu utakaofanyika wakati wowote.
5. Siku ya Soko mwanafunzi anaweza kuomba ruhusa kwa Mlezi (Dean kwenda kutafuta mahitaji maalum sokoni,na nilazima avae sare ya Chuo au T-shirt yenye nembo ya chuo.
6. Mgeni yeyote wa mwanafunzi haruhusiwi kuingia bwenini/Hospital, akae sehemu maalum ya wageni. Baada ya saa 12:00 jioni mgeni haruhusiwi kuwepo kwenye maeneo la Chuo/Hospital na siku za wageni ni Jumamosi na Jumapili tu kuanzia saa 07:00 mchana hadi saa 12:00 jioni.
7. Mwanafunzi atawajibika kufanya usafi {IPC} wa bweni lake, darasa, viwanja vya Chuo/Hospital na sehemu zingine atakazopangiwa na uongozi wa Chuo/Hospitali.
8. Radio na vyombo vya muziki haviruhusiwi chuoni.
9. Kila mwanafunzi atapewa likizo ya siku ishirini na nane (28) au wiki nne (4) kwa mwaka na siku kumi na nne (14) au wiki mbili kabla ya kuanza mwaka mpya wa masomo. Siku ishirini (20) za ugonjwa ndani ya miaka mwili (2) zinakubalika. Siku kumi na nne (14) zaidi ya hapo hatafanya mtihani wa kuhitimu wa Serikali.
10. Mwanafunzi akikosekana majuma matatu (3) mfululizo Chuoni atarudia mwaka.
11. Mwanafunzi akiugua aende kwanza kwa Mwalimu wa Zamu/

Warden ili apewe sick-sheet kabla ya kwenda kwa Mganga. Matibabu ya mwanafunzi ya ziada yatalipwa na yeye mwenyewe kwa kufuata utaratibu uliowekwa.

12. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi wa kike au kiume kuwa na uhusiano wa kimapenzi/uchumba wakati wa masomo, ama sivyo wataachishwa masomo.

13. Mwanafunzi yeyote wa kike atakayepata mimba akiwa masomoni ataachishwa masomo kwa mwaka mmoja, na mwanafunzi wa kiume akijulikana amempatia mwanafunzi mwenzie wa kike mimba pia naye ataachishwa kwa muda wa mwaka mmoja.

14. Kila mwanafunzi lazima shiriki kikamilifu katika shughuli za kujitegemea (self-reliance). Mwanafunzi atakayeonyesha ulegevu, utoro na uzembe katika shughuli hizo atachukuliwa hatua kali.

15. Kila mwanafunzi analazimika kushiriki katika michezo (k.m. mpira) na shughuli za starehe (k.m kwaya, sanaa) kwani ni sehemu ya masomo.

16. Mwanafunzi haruhusiwi kwenda na simu darasani au kazini.

17. Makosa yanayoweza kumwondoa mwanafunzi Chuoni ni kama yafuatayo:

- Uasherati, Ulevi, Utoaji mimba, uvutaji sigara,kutumia bangi au dawa za kulevya ,Matusi, ugomvi na kupigana ,Kutowatii Walimu na Wakuu wa Hospitali,Wizi wa aina yoyote ,Udanganyifu na uongo wa aina yoyote,Kutohudhuria darasani bila sababu maalum

- Kuvunja taratibu, kanuni na sheria za nchi

18. Baada ya kusoma kanuni na sheria za Chuo, hakikisha umeweka saini katika sehemu yako kwenye **kiambatanisho C** hapa chini na mzazi/mlezi wako.

KIAMBATANISHO –C

NAKUBALIANA NA KANUNI/SHERIA ZILIZO KWENYE BARUA YA KUJIUNGA NA CHUO HIKI NA NINA AHIDI KUYATEKELEZA VEMA.

Jina kamili la Mwanafunzi

_____

Saini ya mwanafunzi

_____

Jina la Mzazi/Mlezi

_____

Saini ya Mzazi/Mlezi

_____

Anuani ya Mzazi/Mlezi:

Simu: _____ Email: _____

KARIBU SANA KATIKA CHUO CHA SAYANSI YA AFYA NA TECHNOLOJIA CHATO ILI UPATE ELIMU BORA NA MAFANIKIO

CHATO COLLEGE OF HEALTH SCIENCES AND TECHNOLOGY

OUR MOTTO IS - COMMITMENT TO SUCCESS